# Kurejesha Gharama (Estate Recovery) Huilipa Jimbo kwa ajili ya Matibabu na Huduma na Usaidizi wa Muda Mrefu

**Estate Recovery Repaying the State for Medical and Long-Term Services and Supports**

Kurejesha gharama (estate recovery) ni nini?

- Sheria ya jimbo (sura ya RCW 41.05A na 43.20B) inataka mali yako ilipe Idara ya Huduma za Jamii na Afya (DSHS) na Mamlaka ya Huduma ya Afya (HCA) kwa ajili ya gharama za huduma za matibabu na huduma na usaidizi wa muda mrefi (LTSS) uliopokea.

Mali (estate) ni nini?

- Mali zote na rasilimali nyingine zozote unazomiliki au kuwa na maslahi ya kisheria wakati umekufa zinazorithishwa kwa wosia au bila wosia. Hii hujumuisha mali na rasilimali kama vile:
  - Nyumba, ardhi;
  - Akaunti za benki;
  - Hisa, hatifungani;
  - Mali binafsi; na
  - Rasilimali zenye wanufaika, mali za maisha.

Kitu gani si sehemu ya mali zako?

- Mali au rasilimali nyingine ambazo humilki au kuwa na maslahi ya kisheria wakati wa kifo chako. Kwa mfano, mali au rasilimali nyingine zinazomilikiwa tu na wazazi wako, mwenzi, mpenzi wa kinyumba aliyesajiliwa kisheria, au mtoto.

Rasilimali zipi hazihusiki katika kurejesha gharama?

- Baadhi ya rasilimali za kijadi.
  - WAC 182-527-2746 (6) inaelezea kanuni ambazo ni mahsusi kwa Wahindi wa Marekani na Wazawa wa Alaska. Kanuni hii inaorodhesha rasilimali na mali zinazomilikiwa na Wahindi wa Marekani na Wazawa wa Alaska zisizohusika katika kurejesha gharama. Imechapishwa katika https://app.leg.wa.gov/WAC/default.aspx?cite=182-527-2746.
  - The Northwest Justice Project ina kipeperushi kuhusu WashingtonLawHelp.org kinachoelezea kanuni hii kiitwacho "Native American and Alaska Native Property Owners: Exemptions from Estate Recovery": https://www.washingtonlawhelp.org/resource/exemptions-from-estate-recovery-for-property.
  - Ukihitaji usaidizi wa kupata nakala ya kanuni hii, tafadhali wasiliana na uongozi wa DSHS unaosimamia kesi yako.
  - Ukiwa na maswali zaidi kuhusiana na kurejesha gharama za Wahindi wa Marekani na Wazawa wa Alaska, wasiliana na Ofisi ya Urejeshaji Fedha (OFR) kupitia 800-562-6114.
- Baadhi ya malipo ya fidia za serikali; na
- Rasilimali zinazolindwa na sera ya ubia wa matibabu ya muda mrefu.

Vipi kama huna rasiliamli zozote wakati wa kifo chako?

- Gharama hazitarejeshwa.

Gharama gani za matibabu na LTSS zipo katika kurejesha gharama?

- Gharama za LTSS zinazofadhiliwa na serikali kuu ambazo DSHS au HCA hulipa ukifikisha miaka 55.
- Gharama zinazofadhiliwa na jimbo ambazo DSHS au HCA hulipa katika miaka yoyote, isipokuwa:
  - Huduma za kuwalinda watu wazima:
  - Malipo ya ulinzi wa ziada yaliyoidhinishwa na Usimamizi wa Ulemavu wa Makuzi (DDA),
  - Huduma ya programu ya kuwarejesha wahalifu kwenye jumuiya,
  - Huduma za kazi za wajitoleaji, na
  - Huduma za Programu za Usaidizi wa Utunzaji na Uhifadhi (GCAP).

Gharama gani za matibabu na LTSS hazipo katika kurejesha gharama?

- Gharama ambazo HCA inalipa chini ya Medicare Savings Program.
- Gharama za matibabu ambazo HCA hulipa ikiwa hupokei LTSS.
- Huduma za Usaidizi Maalum kwa Wazee (TSOA).

Lini kurejesha gharama kunacheleweshwa?

- Ikiwa utafariki kabla ya mwenzi wako,
- Ikiwa utafariki na kuacha mtoto chini ya miaka 21,
- Ikiwa utafariki na kuacha mtoto ambaye ni kipofu au mlemavu wakati wa kifo chako, au
- Wakati wa kipindi cha ugumu usio wa lazima, ikiwa mrithi ataomba ucheleweshaji wa ugumu usio wa lazima na DSHS kuidhinisha ombi.

Lini DSHS itaidhinisha ugumu usio wa lazima?

- Kurejesha ghrama humnyima mrithi mahali pa kuishi na hawezi kumudu hifadhi nyingine,
- Mali hiyo ndiyo rasilimali pekee ya kuzalisha kipato cha mrithi, au
- Umefariki na kumuacha mpenzi wa kinyumba aliyesajiliwa kisheria.

Vipi kama unaishi katika kituo cha matibabu na kimantiki hutarajiwi kurudi nyumbani?

- Ingawa si "Kurejesha Gharama," DSHS inaweza kuweka zuio kabla ya kifo (pre-death lien) kwenye nyumba yako kutokana na Sheria ya Usawa wa Kodi na Wajibu wa Kifedha (TEFRA) ya mwaka 2005.
- Sheria inairuhusu DSHS kuweka zuio kwenye nyumba yako kabla ya kifo.
- Watu wanaopaswa kulipia ghrama zao za matibabu ndiyo tu wanaweza kuwekewa zuio kwenye nyumba yao.
- Ikiwa DSHS ina zuio kwenye nyumba yako na ukaiuza, DSHS itarejesha gharama za matibabu na LTSS kutoka kwenye mauzo hayo.
- DSHS haitaweka zuio kwenye nyumba yako ikiwa mwenzi wako, mpenzi wa kinyumba aliyesajiliwa kisheria, mtoto chini ya miaka 21, au ndugu anaishi kwenye nyumba hiyo.
- DSHS itaondoa zuio ikiwa utarudi nyumbani.

Vipi kama unataka taarifa zaidi?

- Piga Nambari ya Uratibu wa Elimu ya Sheria, Ushauri na Rufaa (CLEAR) bila gharama yoyote kupitia 1-888-201-1014.
- Omba ushauri kutoka kwa mwanasheria anayeelewa kanuni za kuweka mipango ya mali na usaidizi wa matibabu.
- Soma "Estate Recovery for Medical Services Paid for by the State" kupitia www.washingtonlawhelp.org.
- Soma sura ya RCW 41.05A na 43.20B na sura ya 182-527 WAC: https://app.leg.wa.gov/WAC/default.aspx?cite=182-527.
- Wasiliana na Ofisi ya Urejeshaji wa Fedha (OFR) kwa maswali ya kurejesha gharama kupitia 800-562-6114.